Stanbic Bank

MAELEZO NA MASHARTI YANAYOHUSU MIKOPO BINAFSI ISIO NA DHAMANA

Maelezo na masharti ambayo yamerejewa humu yanaelezea haki na wajibu kati yako na Benki kuhusiana na Mkopo Binafsi Usio na Dhamana (hapa unarejewa kama “mkopo”). Mkopo unaweza kupatikana ama kupitia (i) maombi kwa makaratasi,(ii) benki kwa intaneti na Chaneli Nyingine. Kwa madhumuni ya maelezo na masharti haya “Chaneli. Nyingine “ina maana ya maombi ya (i) Huduma ya
Data ya Ziada (USSD) Maombi (*150*29//) na/au
(ii) Maombi kwa Simu ya Stanbic kama utakavyojulishwa mara kwa mara.

1. Mrejesho wa Malipo

1.1 Malipo yote unayofanya yawe malipo makuu, riba, ada, gharama au vinginevyo, yatafanywa yakiwa hayana mgogoro, mkato wa deni au madai kinzani na kutokuwa na makato au vizuizi kwa sababu ya kodi au vinginevyo.

1.2 Nyakati zote ni wajibu wako kuhakikisha kwamba fedha za kutosha zinapatikana kwenye tarehe iliyoelezwa kulipa madeni kama ilivyoainishwa katika jedwali la mrejesho wa malipo lililooambatishwa hapa.

1.3 Unaweza kulipa sehemu yote ya deni lililobakia kabla ya tarehe iliyowekwa.

1.3.1 Ikiwa utalipa deni lako kabla ya tarehe iliyowekwa, tozo ya ulipaji mapema itatozwa. Kima kinachohusika kinaonyeshwa katika kiongozi cha ushuru kilichochapishwa na Benki.

1.4 Ingawa ni hivyo Benki inaweza kukuruhusu kupunguza bakaa la deni kwa malipo ya kila mwezi kama ilivyoonyeshwa katika jedwali la mrejesho wa malipo kadiri itakavyorekebishwa mara kwa mara. Makato ya kila mwezi yanayolipwa na wewe haina maana kwamba deni hilo litakuwa limelipwa lote katika kipindi cha awali cha muda wa mkopo huo, kutokana na kutoa pesa na/au malipo yanayofanywa na wewe katika akaunti ya mkopo na/au mabadiliko ya kima cha riba yanayotumika mara kwa mara.

1.5 Unaahidi kwamba mkopo utalipwa wote ikiwa utahamisha akaunti yako benki nyingine.

2. Riba

2.1 Riba ya kulipwa kuhusu deni

2.1.1 itakokotolewa kwa msingi wa siku 365 kwa mwaka, kwa mikopo ya shilingi za Kitanzania na siku 360 kwa mwaka kwa mikopo kwa fedha za kigeni bila kujali kwamba mwaka unaohusika ni mkubwa;

2.1.2 ongezeka siku hadi siku;

2.1.3 itakatwa kutoka akaunti yako ya mkopo kila mwezi kwa viporo; na

2.2 Viwango vya riba vilivyoonyeshwa au kuamuliwa awali au kubadilishwa baadaye na Benki vinahusu matumizi ya mikopo katika ukomo uliokubaliwa na Benki kwa maandishi. Madeni yoyote ya Benki kwa zaidi ya ukomo uliokubaliwa na Benki kwa

maandishi unaweza kutozwa riba kubwa zaidi kadiri Benki itakavyoamua kwa hiari yake wakati ambapo deni limepatikana na/au muda wowote baadaye. Kiwango hiki hakifanyi mkataba na Benki kuruhusu mikopo zaidi ya kiwango cha mkopo ulioidhinishwa.

2.3 Kiwango cha riba cha kulipwa kuanzia tarehe ambayo mkopo umetolewa kwako kama inavyoonyeshwa katika jedwali la malipo kama ambavyo inaweza kurekebishwa mara kwa mara kwa maelezo na masharti yaliyoambatanishwa.

2.4 Benki inaweza, mara kwa mara kubadilisha viwango vya riba vinavyotumika kwenye mkopo wako ikiwa Kiwango cha Ukopeshaji cha Benki kinabadilika katika kipindi kilichokubaliwa cha mkopo wako. Kwa mujibu wa ibara hii “Kiwango cha Ukopeshaji cha Benki” ni kiwango cha chini cha riba kwa mwaka kilicho chapishwa ambacho Benki hutolea mikopo mara kwa mara. Benki ina haki ya kurekebisha kiwango cha riba na namna ya kukikokotoa kwa muda unaohusika kulingana na hali ya soko au mazingira yaliyoainishwa kwenye ibara ya 3. Benki itakupatia taarifa ya siku thelathini kabla ya kufanya mabadiliko.

2.5 Iwapo pesa zozote unazodaiwa hazitalipwa inapotakiwa Benki itakuwa na haki ya kutoza riba ya ukiukaji asilimia kumi (10%) kwa mwaka pamoja na kima cha riba unapotenda tukio lolote ya ukiukaji katika aya ya 8 hapa chini. Unaridhia kwamba kiwango cha riba ya ukiukaji kilichoainishwa hapa ni kidario sahihi la hasara ya Benki ambalo litatumika (kwa hiari ya Benki pekee) kutokana na ukiukaji wako wowote.

3. Mabadiliko katika Mazingira

3.1 Bila kuathiri chochote kilicho katika mkataba huu, mabadiliko yoyote katika kuanzishwa kwa sheria, kanuni, uamuzi, amri, sera na/au miongozo au tukio lolote ambalo kwalo Benki au kitengo chake chochote inabidi kutekeleza na/au ni kwa mujibu wa utendaji wa benki yoyote, au tafsiri yoyote ambayo utekelezaji wake unasababisha ongezeko lolote kwa Benki katika gharama za uendeshaji na/au utoaji wa mkopo au sehemu yoyote ambayo haijatumiwa, Benki ina haki ya kufidia gharama hizo za ziada kutoka kwako.

3.2 Mazingira ya hapo juu yanajumlisha (bila ukomo) Mchafuko wa Soko. Kwa mujibu wa ibara hii “Mchafuko wa Soko” unajumlisha mazingira ambapo gharama kwa Benki katika mkopo kutoka chanzo chochote inachoweza kuchagua kinazidi Kiwango cha Chini cha Ukopeshaji cha Benki. Katika mazingira kama hayo kiwango cha riba kitakuwa Kiwango cha Chini cha Ukopeshaji cha Benki na gharama za benki za kulipia mkopo huo kutoka chanzo chochote inachoweza kuchagua.

4. Masharti ya Awali

Kwa kuzingatia Benki kutoa mkopo unaahidi kuhakikisha utekelezaji wa masharti ya awali kwa kuitosheleza Benki:

4.1 kuwasilisha nakala ya mkataba huu wa mkopo kuridhia maelezo na masharti yaliyoainishwa hapa.

4.2 malipo ya ada ya uwezeshaji; na

4.3 umeweka kinga za bima ya kutosha kadiri inavyoweza kutakiwa na Benki kutoka kwa Mtoaji Bima wa Benki ambapo Benki inawekwa kama mlipwaji wa kwanza wa hasara.

4.4 Benki inathibitisha kwako kwamba hakuna Kushindwa Kiuchumi. Kwa mujibu wa ibara hii "Kushindwa Kiuchumi" ina maana kuwa kwa maoni ya kawaida ya Benki, ni kutokea kwa mabadiliko au mdororo wowote nchini au kimataifa katika mtaji, pesa, benki, kiuchumi, kisiasa au masharti ya hali ya fedha sokoni wakati wowote, kutoka na kujumlisha tarehe ambayo maelezo na masharti ya mkataba huu wa mkopo yanakubaliwa na wewe mpaka (na kujumlisha) tarehe ya utekelezaji wa Masharti ya Awali ambayo inaifanya Benki kutoweza au kutokuwa na faida kutoa mkopo kwa vyovyote au kwa maelezo na masharti yaliyoainishwa katika mkataba wa mkopo.

5. Hati ya Deni

Kiasi cha deni lako kwa wakati wowote ule na kwamba kudaiwa huko (pamoja na riba yoyote na kiwango ambacho riba inakokotolewa) kumefika muda wake, kunaweza kuamuliwa na kuthibitishwa na hati inayoonyesha hivyo ambayo imetiwa saini na ofisa yeyote wa Benki aliyeidhinishwa, ambaye ajira na mamlaka yake ya kutia saini hakuhitaji kuthibitishwa. Hati hiyo itatosha kuwa ithibati ya mambo yaliyoandikwa ndani yake.

6. Mapato

Unaahidi kuwa na akaunti ya hundi na sisi ambako mshahara wako utaingizwa .

Unaahidi kuwa haraka utatoa maelekezo ya maandishi yasiyopingika kwa mwajiri wako (maelekezo ambayo yatatiwa saini na wewe na kunakiliwa kwa Benki) ukiwaelekeza kuweka mshahara wako au mapato katika akaunti yako miamala au ya hundi katika vitabu vya Benki.

Bila pingamizi unairuhusu Benki kutoa kwenye akaunti hiyo makato ya kila mwezi yanayorejewa katika jedwali la mrejesho malipo kama itakavyo rekebishwa mara kwa mara na katika mkataba wa mkopo pamoja na ada zozote za Benki za mwezi na tozo zinazohusika. Maelezo hayo yatabaki mpaka Benki itakapoamuru ufutwaji. Katika kipindi cha mkopo huu unaahidi

kuwa hutafanya maelekezo ya malipo kinzani bila ya idhini ya maandishi ya Benki.

7. Kipindi cha Mpito

Unastahili kipindi cha mpito cha siku kumi mara tu baada ya kutia saini mkataba wa mkopo, alimuradi huchukui pesa hizo. Katika kipindi hicho cha mpito unaweza kuvunja mkataba wa mkopo bila ya kupewa adhabu yoyote.

8 Ukiukaji na Uvunjaji

8.1 Benki haitawajibika kufanya uhawilishaji au kuzungusha kiasi chochote katika mkataba na Benki inaweza kugeuza mkopo kuwa ule ambao unaweza kulipwa baada ya kutakiwa na/au Benki inaweza kupitia maelezo au masharti yoyote na kuongeza kiwango cha riba kinachotozwa endapo ukiukaji wowote hapa chini unatokea:

8.1.1 unakiuka maelekezo au masharti yoyote ya mkopo au mkataba mwingine wowote kati yako na Benki na unashindwa kurekebisha ukiukaji huo ndani ya siku 7 baada ya kupewa taarifa ya maandishi kufanya hivyo;

8.1.2 unashindwa kulipa makato yanayotakiwa kwa mujibu wa mkataba wa mkopo;

8.1.3 Benki inaona kuna mdororo mkubwa wa hali yako ya kifedha au uendeshaji wa akaunti yako ya muamala;

8.1.4 maelezo au uthibitisho wowote uliofanywa kuhusiana na mkopo au nyaraka zozote zilizoletwa na wewe, kwa maoni yetu, sio sahihi, havikukamilika au zinapotosha;

8.1.5 mchakato umeanzishwa kukutangaza wewe muflisi au amri ya muda au ya mwisho imepitishwa kukutangaza kuwa muflisi au maridhiano au mpango wowote kati yako na wadai wako vinaidhinishwa au kutekelezwa au.

8.1.6 hati ya utekelezaji imetolewa na mahakama yoyote yenye mamlaka kukamata mali zako zozote;

8.1.7 mshahara au malipo hayapitishwa Benki kwa sababu yoyote;

8.1.8 kwa jumla hutafanya au kuacha kufanya kitu chochote ambacho kinaweza kuathiri haki zetu kwa mujibu wa mkopo au kufanya kupata hasara au uharibifu wowote; au

8.1.9 unaacha kuwa mfanyakazi wa kampuni au asasi; na

8.2 Katika matukio yoyote yanayotazamiwa katika ibara ya 8.1, Benki itakuwa na haki, bila kuathiri haki nyingine au taratibu nyingine ambazo ziko wazi kwa Benki kukatisha mkopo na kudai mara moja marejesho ya bakaa iliyobaki au katika tarehe iliyotajwa katika taarifa yoyote. Endapo mkopo utakatishwa fedha zozote ambazo zinadaiwa na Benki zitalipwa:

8.2.1 mara moja, ikiwa imeelezwa katika taarifa; au

8.2.2 kwenye tarehe iliyotajwa katika taarifa.

9 Makato Deni na Ulipaji

9.1 Ikiwa kutatokea ukiukaji, Benki inaweza, wakati wowote bila ya

taarifa ya ziada kwako, na bila kujali kiasi na ulipaji wowote mwingine, kuunganisha akaunti zako zote au ambazo ziko Benki, pamoja na zile ambazo ziko kwa jina la Benki au wewe peke yako na kukata deni au kuhamisha kiasi chochote kilichobaki kwa ajili ya akaunti moja au nyingine katika kutekeleza dhima yoyote au deni lako kwa Benki, dhima hiyo iwe ya sasa, baadaye, dhahiri, (tegemevu), dhamana, pekee au kwa pamoja na unaachia haki ya kukata deni inayoweza kuwa nayo kwa mujibu wa sheria. Benki itatoa taarifa ya chapisho kwa mkopaji baada ya kukata deni.

9.2 Dhamana yoyote iliyowekwa inaweza kuchukuliwa kufidia deni lako lolote kwenye Benki, kwa hiari yake bila kujali kuwa kudaiwa huko kuko katika fedha tofauti na ile ambayo hutumika na Benki kulipa deni.

10. Gharama

10.1 Bila kizuizi unaidhinisha Benki kukata akaunti yako ya hundi/ muamala na kufidia (iwe au isiwe mkopo umetolewa) ada zote za kisheria na gharama nyingine zinazopatikana (pamoja na tozo ya stempu na kodi ya ongezeko la thamani) ambazo Benki inapata kutokana na utendaji au upunguzaji wowote wa dhamana (kama upo) au utekelezaji au uhifadhi wa Benki wa haki zake chini ya mkataba huu au marekebisho yoyote yanayohusika.

10.2 Utalipa ada, gharama na tozo zote zinazorejewa katika mkataba huu na ada, gharama, tozo na kodi zote ambazo Benki inaweza kuzipata au kulipa kuhusiana na maandalizi, ukamilishaji au utekelezaji wa mkataba pamoja na:

10.2.1 Gharama za kisheria, pamoja na gharama baina ya wakili na mteja wetu, ushuru wa ukusanyaji, ada za ufuatiliaji na ada nyingine au malipo yanayofanywa katika ukosanyaji au katika kufanya ukusanyaji wa fedha zote au sehemu yake ambazo zinadaiwa na Benki pamoja na kodi ya ongezeko la thamani pale inapotakiwa;

10.2.2 Nyongeza yoyote katika ada na gharama kama inavyoamuliwa na kuchapishwa mara kwa mara;

10.2.3 Ada na tozo nyingine zozote zitalipwa kwa mujibu wa kiongozi cha ushuru wa forodha kilichochapishwa na Benki na kurekebishwa mara kwa mara. Kiwango kinachotumika kinaweza kutolewa kwako kwa maombi;

10.2.4 Ada ya kuanzia ni ada ya mara moja inayotumika kwa mikopo yote, inayotozwa kwa mujibu wa kiongozi cha ushuru wa forodha kinachochapishwa na Benki ambacho kinaweza kubadilika mara kwa mara na kinalipwa kwanza baada ya ithibati ya mwisho ya Benki. Kiwango kinachotumika kinaweza kutolewa kwako kwa maombi;

10.2.5 Ada inayozunguka inaweza kutozwa kuhusiana na mikopo yote inayozunguka kwa mujibu wa kiwango cha ushuru wa forodha kilichochapishwa na Benki. Tozo ya kila mzunguko ulioidhinishwa itakatwa kutoka akaunti yako ya

muamala. Kiwango kinachotumika kinaweza kutolewa kwako kwa maombi.

11. Kinga ya Mkopo

11.1 Benki inataka mikopo yote kuwa na kinga ya mkopo ya kutosha kusalimisha mkopo wako wakati wa kifo, ulemavu wa kudumu na kuachishwa kazi. Kinga ya mkopo pia inatoa mafao ya mazishi utakapo kufa.

11.2 Unaridhia Benki kupata kinga ya mkopo.

11.3 Bakaa la mkopo mkuu kwa kifo na ulemavu wa maisha litalipwa lote bila karisaji. Mawanda ya kinga ni kama ifuatavyo: 11.3.1 Kifo

11.3.1 Kifo

(i) Kifo kinachotokana na ajali au ugonjwa ambao haukujulikana kwa miezi 6 iliyopita;

(ii) Kwa hali au ugonjwa uliokuwepo, muda wa kusubiri wa miezi 3 utahitajika; na

(iii) Kujiua kutasubiri miezi 12.

11.3.2 Ulemavu wa Kudumu

(i) Kushindwa kutukutumia mikono au miguu yote;
(ii) Kushindwa kutumia mkono au mguu mmoja;
(iii) Kushindwa kuona kwa macho yote; na
(iv) Ugonjwa au ajali yoyote ambayo inakusababishia ulemavu wa kudumu.

11.3.3 Kuachishwa Kazi

Unapoachishwa kazi bila hiari utalipwa malipo ya mkopo kila mwezi kwa kipindi cha miezi kumi alimuradi iwe hukupata ajira nyingine au njia nyingine ya malipo. Sharti uwe umelipia mkopo sio chini ya miezi 6 kutoka siku ya malipo.

11.3.4 Mazishi

Mafao ya kinga ya mazishi yanatolewa katika akaunti ya akiba. Ni wajibu wako kuwashauri warithi wako kuhusu mafao ya maziko ili waweze kudai. Utakapo kufa mafao ya mazishi yataingizwa katika akaunti yako.

Maelezo na masharti mengine yatatumika kwa mujibu wa sera ya kinga ya mkopo.

11.4 Gharama ya kinga ya mkopo itakuwa kwa hiari ya Benki pekee ama ikatwe kutoka kiasi cha mkopo baada ya malipo au kuwekwa kwenye malipo ya mwezi. Kinga ya bima ya mkopo inatumika hadi unapomaliza kulipa deni lako. Utapewa nakala ya kinga ya bima ya mkopo yenye maelezo na masharti yake.

12. Mikopo ya fedha za kigeni

Endapo yatatokea mabadiliko ya kisheria au mabadiliko makubwa katika mazingira ya soko yatakayo athiri uwezo wa benki kutoa au kulipia mikopo kwa fedha za kigeni, Benki inabaki na haki, kwa hiari yake yenyewe, kubadilisha deni lolote lako kwa fedha za kigeni kuwa fedha za Tanzania kwa kiwango kinachotumika siku ya

mabadiliko hayo. Aidha, endapo Benki inadaiwa malipo ya deni hilo, Benki ina haki, kwa hiari yake yenyewe, kubadilisha deni lako la fedha ya kigeni kwa shilingi ya Tanzania kwa kutumia kiwango cha siku hiyo ya mabadiliko. Katika utekelezaji wa haki hizo za kubadilisha madeni yako kwa fedha za kigeni kwa fedha ya Tanzania, Benki haitahusika na hasara yoyote inayotokana na mabadiliko ya viwango hivyo.

13. Mabadiliko

Tunaweza kubadilisha, kurekebisha, kuongeza au kuondoa masharti haya wakati wowote kwa kukupatia taarifa isipokuwa pale ambapo marekebisho hayo yanasababisha athari hasi kwako. Marekebisho yoyote kwenye maelezo na na masharti ya mkataba huu yatafanya (version) mpya ya maelezo na masharti mapya ambayo yata kubadilisha (sura) ya zamani na kukubana wewe na sisi kutoka tarehe ambayo imeonyeshwa kwenye tangazo. Mabadiliko yoyote ya riba yatawasilishwa na Benki kwako kwa maandishi.

14. Majanga Asili

Benki haitawajibika kwa kushindwa kutekeleza majukumu yoyote humu yanayotokana na sababu nje ya uwezo wetu moja kwa moja au sio moja kwa moja kutokana na kutenda au kutotenda kwa serikali, mamlaka yoyote ya serikali, fujo, migomo, mapinduzi, vizuizi, uasi wa kiraia, kadari ya Mungu, mabadiliko katika sheria au mabadiliko makubwa katika hali ya soko. Benki itakujulisha mapema kupitia njia mbalimbali, pamoja na ujumbe mfupi, barua pepe, barua au taarifa kwenye ATM, kwenye matawi yetu na njia nyingine ambazo zitakuwa lazima kutumika kwa nyakati tofauti.

15. Utoaji

Hutakuwa na haki ya kuhawilisha haki, wajibu au maslahi yao yoyote au sehemu yake hapa bila ya ridhaa ya maandishi ya Benki.

16 Makubaliano ya jumla

16.1 Wakati mikopo inapatikana unaahidi kwamba:

16.1.2 Majukumu yako kuhusiana na mikopo nyakati zote sharti yawe japo sawa kwa sawa na majukumu yote ya sasa na baadaye yaliyodhaminiwa;

16.1.2 Mara baada ya kupata taarifa mara moja utaiarifu Benki kuhusu kuwepo kwa shauri lolote la msingi, upatanishi au mwenendo wa kiutawala ambavyo vipo, au kwa kadiri ya uelewa wako, taarifa iliyotolewa dhidi yako ambayo inaweza kutishia uwezo wako wa kutekeleza maelezo au masharti yoyote katika mkataba huu.

16.1.3 Ikiwa kutatokea mabadiliko ya ajira sharti uifahamishe Benki kuhusu mwajiri wako mpya na kuamuru uendeleaji wa makato ya kila mwezi kutoka mshahara wako mpya kwa mujibu wa masharti ya mkataba huu.

17 Utenganishi

Kila kipengele cha mkataba huu wa mkopo kinajitegemea. Iwapo wakati wowote kipengele chochote kinakuwa au kinagundulika na mahakama yenye mamlaka kamili, batili, hakifai, kimekosewa au hakitekelezeki kwa sababu yoyote ile, vipengele vingine vilivyosalia vitakuwa na nguvu na matumizi kamili.

18 Sheria ya Kutumika na Mamlaka

Mkataba huu wa mkopo utasimamiwa na kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania na mahakama ya Tanzania yatakuwa na mamlaka ya kutatua migogoro yoyote inayoweza kutokea kuhusiana nao bila kuathiri haki ya Benki kufungua mashauri dhidi yako kwenye mamlaka nyingine yoyote.

19 Taarifa za Siri na Ulinzi wa Data

19.1 Katika ibara hii ya 19; marejeo kwa:

19.1.1 **Taarifa Binafsi** ina maana ya taarifa kuhusu mtu halisi anayeweza kutambulika, na pale inapohusika, mtu kisheria, pamoja na, lakini sio pekee, taarifa pia kuhusu: mbari, jinsia, mimba; hali ya kindoa, utaifa, usuli wa kikabila; rangi; usuli wa mazingira ya kijinsia, hali ya kimwili au akili, uwezo kimali, ulemavu, dini, imani; utamaduni; lugha; uzawa, elimu, tiba; fedha, historia ya ajira, namba yoyote ya utambuzi; alama, barua pepe, anuani ya posta au mtaa, mahali; namba

yoyote ya utambulisho, barua pepe, namba ya simu, mahali, kitambulisho chochote kingine cha kipekee; kazi nyingine yoyote ya mhusika, taarifa ya kibaiometriki, maoni binafsi, maoni au utashi wa mhusika; msimamo au maoni ya mtu mwingine kuhusu mhusika; mawasiliano yaliyotumwa na mhusika ambayo dhahiri au kiufahamifu yana silka ya kibinafsi au siri au mawasiliano ya ziada ambayo yatafichua mawasiliano ya awali; na jina la mtu linaloonekana na taarifa nyingine binafsi kuhusiana na mtu huyo au kutangaza jina lake pekee kutafichua taarifa ya mtu huyo.

19.1.2 Mchakato una maana ya kitendo chochote kinachojiendesha au la kuhusu Taarifa Binafsi, urekebishaji, ukusanyaji, ushauri, ushushaji, uharibifu, utoaji taarifa kwa njia ya usambazaji au kufanya ipatikane kwa namna yoyote,ufuataji, ulinganishaji, upangaji, upokeaji, kurekodi, kuchukua, kuhifadhi, kuboresha, kurekebisha au matumizi ya taarifa. Utumiaji na iliyotumika itakuwa na maana moja.

19.2 Unatupa ridhaa kukusanya Taarifa yako Binafsi kutoka kwako na, iwapo ni halali na inafaa , kutoka vyanzo vya umma kuhusu mikopo, udanganyifu na

madhumuni yaliyoainishwa hapa chini.

19.3 Iwapo utatupa Taarifa Binafsi kuhusu au kwa niaba ya watu wengine (pamoja na wenye saini katika akaunti, wenye hisa , maafisa watendaji wakuu, wadhamini na wanufaishwa) unathibitisha kwamba unaidhinisha (a) kutupatia Taarifa Binafsi; (b) kuridhia kwa niaba yao kwa utumiaji wa Taarifa zao binafsi hususan upelekaji wowote wa Taarifa ndani au nje ya nchi ambako bidhaa na huduma zinapatikana; na (c) kupokea taarifa binafsi zozote kwa niaba yao.

19.4 Unatupa ridhaa ya kutumia Taarifa yako Binafsi:

19.4.1 Kukupatia bidhaa na huduma kwa mujibu wa mkataba huu na kukupatia bidhaa nyingine na huduma unazoweza kuomba;

19.4.2 Kufanya uchambuzi wa kitakwimu na mwingine ili tuweze kutambua masoko muhimu na mwendo wake, kutathmini na kuboresha biashara yetu (hii inajumlisha kuboresha na kuendeleza bidhaa na biashara mpya);

19.4.3 Kwenye nchi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Nchi hizi zinaweza zisiwe na sheria sawa za ulinzi wa data kama nchi ambayo bidhaa na huduma zinatolewa. Tunapoweza tutamuomba mhusika anayepokea kuafiki sera zetu binafsi;

19.4.4 Kwa kutumia pamoja Taarifa yako Binafsi na watoaji wetu huduma wengine, ndani na nje ya nchi ambako bidhaa na huduma zinatolewa. Tunaomba watu wanaotoa huduma kwetu kukubali sera zetu iwapo wanahitaji kutumia Taarifa Binafsi yoyote kufanya shughuli zao; na

19.4.5 Ndani ya Kundi.

19.5 Unatambua kuwa tunatakiwa na sheria mbalimbali kukusanya sehemu ya Taarifa yako Binafsi na unaridhia kutumia taarifa hii na sisi:

(i) Utapata taratibu za utumiaji wetu katika maelezo ya Kundi na yetu binafsi. Maelezo haya yanapatikana katika tovuti ya Kundi au kwa maombi.

(ii) Ikiwa huna hakika na hali ya kodi au sheria kwa kuwa Taarifa yako Binafsi inatumika katika nchi mbali na unayoishi, pata ushauri binafsi.

19.6 Utafutaji Masoko

(I) Hapa unaridhia kwa Benki kutumia data na taarifa yako ya siri ndani ya Kundi iwapo ni lazima kwa madhumun ya utoaji huduma kwako.

(ii) Tunaweza kutumia Taarifa yako Binafsi kukueleza kuhusu bidhaa, huduma na ofa maalumu kutoka kwetu au kampuni ambazo zitaweza kukuvutia. Tutafanya hivi kupitia baruapepe, ujumbe wa maandishi (SMS), mitandao ya kijamii au kukuarifu kwenye maombi yako ya simu ya kiganjani.

Iwapo baadaye unaona hutaki sisi kufanya hivi, tafadhali wasiliana nasi kupitia mtandao wetu wa huduma kwa wateja kusitisha huduma hii.

20. Kipengee cha Ridhaa ya Mkopaji

20.1 Kwa kukubali mkataba huu wa mkopo, Mkopaji anakubali na kuiruhusu Benki;

20.1.1 kufanya uchunguzi kutoka benki yoyote, asasi ya kifedha, Chama cha Benki cha Tanzania ("CRB")kilichopewa leseni na Benki Kuu ya Tanzania kuthibitisha taarifa yoyote iliyotolewa na Mkopaji.

20.1.2 kutafuta taarifa kutoka Benki yoyote, asasi ya fedha na TBA, CRB wakati wa kutathmini akaunti ya Mkopaji.

20.1.3 kufichua kwa TBA,CRB, benki yoyote na asasi ya fedha taarifa yoyote kuhusu akaunti za Mkopaji zinazohifadhiwa na benki zitapoulizwa

20.1.4 kutoa taarifa zote kwa TBA na/au CRB kuhusiana na akaunti zilizopo katika Benki baada ya ukiukaji na/au wakati wa kesi mahakamani;

20.2 bila kuathiri ujumbe wa aya zilizopita, Mkopaji anashauriwa kuelewa maudhui ya kanuni za Kanuni za Rejea za Mikopo za Benki Kuu ya Tanzania Za 2012 (GN Na.416 ya 2012, kadiri itakavyorekebishwa mara kwa mara) kuhusiana na aya ya 20 (Kipengele cha Ridhaa ya Mkopaji).

20.3 Mkopaji ana haki ya-

20.3.1 kujua aina ya taarifa itakayotolewa au kutolewa katika mfumo rejea wa mkopo.

20.3.2 kujua ripoti zao za mkopo;

20.3.3 kuomba nakala ya bure ya taarifa yao ya mkopo mara moja kila miezi kumi na mbili, na

23.3.4 kupinga taarifa iliyopo kwenye ripoti ya mkopo.

20.4 Unakubali bila kipingamizi, kwa Benki kuwasiliana moja kwa moja na mwajiri wako yeyote wa sasa au baadaye kuhusiana na usimamizi na ulipaji wa mkopo.

21. Haki ya kufikisha Malalamiko Benki na kupeleka Benki Kuu ya Tanzania malalamiko ambayo hayakutatuliwa

21.1 Utaratibu wa kufikisha malalamiko unaweza kupatikana kwenye tovuti ya Benki na kila tawi la Benki.

21.2 Kuifanya iwe ya ufanisi kadiri inavyowezekana, zifuatazo ni njia za kupeleka malalamiko kuhakikisha yanasikilizwa:

(i) Tembelea tawi lolote la Benki na zungumza na mfanyakazi wake;

(ii) Wasilisha malalamiko yako mtandaoni kwa tanzaniaccc@stanbic.com.

(iii) Piga simu Kituo cha Mawasilano na Wateja namba ya bure 0800 751111 au;

(iv) Weka malalamiko yako kwa maandishi na yatume kwa posta kwenda:

Meneja CCC
Benki ya Stanbic Tanzania Limited
Kituo cha Stanbic
Kitalu 99A
Kona ya Ali Hassan Mwinyi/ Barabara ya Kinondoni
SLP 72647
Dar es Salaam

21.3 Iwapo malalamiko yako hayatatatuliwa ndani ya muda wa kushughulikia malalamiko ya wateja kama ulivyoainishwa katika Kanuni za Ulinzi wa Watumiaji wa Huduma za Kifedha za Benki Kuu ya Tanzania (Bank of Tanzania Financial Consumer Protection Regulations), unaweza kuwasilisha malalamiko yako kwa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kuandika kwa:

Benki ya Tanzania
Dawati la Utatulizi wa Malalamiko
Ofisi ya Katibu wa Benki
2 Mtaa Mirambo
SLP 11884
Dar es Salaam